

JARIDA LA ATD DUNIA YA NNE TANZANIA

August 2018

"Popote pale wanaume kwa wanawake wanapolazimika kuishi katika maisha ya umaskini uliokithiri, haki za binadamu hukiukwa. Sote ni wajibu wetu wa dhati kujiunga pamoja na kuhakikisha kwamba haki hizi zinaheshimika".

- Joseph Wresinski (1917-1988), founder of ATD Fourth World -



Tahariri



Ndugu wapendwa,

Kama ilivyoonyeshwa katika jarida letu la hivi karibuni, mradi wetu wa utafiti unaoendelea juu ya umaskini (unaogusa nyanja mbali mbali), kuititia mikutano na mijadala na watu wanaoishi katika umaskini na wadau wengine, umeonyesha wazi kwamba, uhalisia wa kiwango cha umaskini uliokithiri unaweza kutazamwa katika sura na vipengele mbali mbali.

Mwezi wa sita mwaka huu, watoto ndio walikuwa kii ni katika kazi za nje katika mradi huu. Kwa makubaliano maalum, walituelezea jinsi wanavyonyimwa haki zao za msingi kama kutokuwa na muda wa kutosha kufurahia utoto wao na changamoto za kupata elimu inavyoweza kuboresha uwezekano wao wa kutotambua uwezo wao wa kupambana na magumu katika maisha yao ya baadae wakishakuwa watu wazima.

Katika Mwezi wa sita, Watu wanne wawakilishi kutoka ATD Tanzania walishiriki katika semina ya kimataifa iliyofanyika makao makuu ya shirika la ATD Dunia ya Nne yaliyoko, Pierrelaye nchini Ufaransa, iliyohusisha washiriki kutoka nchi kumi na nne duniani. Lengo la semina hiyo lilikuwa ni kubadilishana ujuzi na uzoefu wa 'kjifunza kutoka katika mafanikio' ili kuelewa kwa ufasaha mambo ya msingi kwa elimu yenye mafanikio kwa kila mtu, ikiwa ni pamoja na watoto wanaoishi katika umaskini uliokithiri. Tazama jinsi wawakilishi wetu walivyoshiriki.

Simulizi zenye kuleta mabadiliko, ni mpango wa ATD katika kampeni ya kutokomeza umaskini mwaka 2017, ilimshirikisha mwanachama mmoja kutoka ATD Dunia ya Nne Tanzania, Reuben. Simulizi ya Maisha yake, iliyoelezewa hapa, inaelezea jinsi watu wakiungana pamoja kuititia ushirikiano wa wanakijiji ulivywawezesha jamii nzima kupata maendeleo.

Katika kuonyesha umuhimu wa elimu, Jarida letu ililishirikisha mpango wa watu wazima kupata fursa ya kujuu kusoma na kuandika ulioandalisha na ATD katika eneo la Tandale jijini Dar es Salaam na jinsi ilivyo wawezesha kundi la wanaojifunza kuibua vipaji vyta kusoma na kuandika. Na matokeo yake, walijifunza sasa wanajisikia kuwajasiri na huru, kwa kuweza kufanikiwa kupata hatua binafsi ya kuwawezesha kupambana na maisha ya kutengwa katika jamii na kuitokemeza kabisa hofu ya kunyanyasika.

Tunatumaini utafurahia kusoma Jarida letu.

Laurent Ganau, ATD Dunia ya Nne Tanzania..

**Mradi wa utafiti wa kubaini wipimo
vya umaskini na jinsi ya kuvipimo
watoto wanazungumza, Kilimanjaro,
mwezi wa Saba 2018**



Mkoa wa Kilimanjaro ndio uliokuwa eneo la hivi karibuni kwa utafiti uliofanya na kundi la wanachama kutoka ATD Dunia ya nne kama sehemu ya ATD Dunia ya nne katika mradi wa utafiti wa umaskini kimataifa. Utafiti ulitekelezwa kwa ushirikiano wa Manispaa ya Moshi na Wilaya ya Hai vijijini, ambapo timu ilikutana na watoto kutoka shule ya msingi Mwereni na shule ya msingi Mkalama. Jumla ya watoto 8 (4 wavulana na 4 wasichana) katika kila shule zilizotajwa walikutana katika makundi rika na majadiliano yalifanyika kwa zaidi ya siku 3. Watoto walikuwa wenye umri kati ya miaka 9 na 14.

Watoto waliongea juu ya umaskini ulio kithiri wanavyoolewa wao, wakibusiha mada na jinsi familia zao zinavyoishi, majirani na wanafunzi wenzao walivyopitia maisha ya umaskini moja kwa moja. Walielezea umaskini kwa namna mbali mbali, mfano kusafiri umbali mrefu kwenda kufuata shule, kukosa usafiri wa kuwawezesha kuhudhuria masomo na kujikimu, kukabiliana na uhaba wa chakula katika familia, na kuishi na nguo zilizochakaa na kutokuwa na viatu vizuri vya kuvaa.

Watoto walisisitiza juu ya umuhimu wa hali za familia zao. Mara nyinyi wazazi wanatengana na kupelekea mtoto kwenda kuishi na ndugu amba moja kazi za magumu na wakati mwininge mtoto hufanyiwa vitendo vibaya. Kwa mfano, anaweza kulazimika kufanya kibarua na kupeleka pesa nyumbani, au kufanya kazi za nyumbani mara kwa mara au kufanya kazi ngumu za shamba na kukosa muda wa kujisomea na kuhudhuria masomo shulen. Katika mazingira hayo, watoto wengine huishia kwenda mitaani, wasio na mahali pakushi na kuwa katika mazingira hatarishi.

Maelezo kama hayo juu ya umaskini uliokithiri yana athiri moja kwa moja katika haki za mtoto kama iliyoelezewa na Umoja wa Mataifa katika mkataba wa haki ya mtoto. Katika hali ya kawaada, watoto wanaoishi katika umaskini uliokithiri wanavyonyimwa haki zao za kufurahia utoto wao na wako hatarini kuishi katika hali ya umaskini na kutengwa wanapokuwa watu wazima.

Kila kitu tunachopanga kufanya, kinawezekana

Na Jean Venard

Tovuti ya harakati za Kimataifa za ATD Dunia ya Nne, inaeleza hadithi zinazoonyesta kuwa umasikini unaepukika na kwamba pamoja tunaweza kuuzuia umasikini. Jean Venard, mfanyakazi wa kujitolea kwa muda wote na mjumbe aliyepita wa Ukanda wa Afrika alieleza hadithi ya Reuben, mwanachama wa ATD dunia ya nne nchini Tanzania.

<https://bit.ly/2vua0Nu>

Katika kijiji cha Kusini Magharibi mwa Tanzania, Reuben, mwanachama wa ATD Dunia ya Nne, ni mfano hai wa maendeleo yaliyojikita katika ufahamu wa wakazi na uwezo wao wa kuunganisha nguvu pamoja.

Sehemu ya ari ya Reuben katika kupambana na umasikini bila shaka inatokana na ujuzi wake binafsi. Anakumbuka wakati alipokuwa kijana, watu wote waliokuwa wakirejea kutoka Dar es Salaam, jiji kubwa linalopakana na bahari, lenye umbali wa masaa kumi na mbili kutoka kijiji ni kwake Reuben, ambao walikuwa wakisema kuwa kila kitu huko kilikuwa kizuri. Siku moja aliondoka pia kwemda kwenye jiji hilo kubwa na akaishia kufanya kazi ngumu kama kibarua katika maeneo ya ujenzi kwa malipo ya shilingi mia tatu za kitanzania kwa siku, kiasi kwamba ikawa ngumu kulipia chakula chake cha jioni.

Akaamua kusonga mbele. Akawa hali chakula kila siku ya tatu, ili aweze kununua tiketi ya kucheza bahati nasibu. Je, angeweza kuwa mshindi wa shilingi milioni iliyokuwa zawadi kuu? Ama zawadi ya pili ya nusu milioni? Au hata kama ya tatu ya shilingi laki mbili na hamsini elfu?

Visit the webpage

STOP POVERTY
Stories of Change


<https://storiesofchange.atd-fourthworld.org/>
and discover many others stories from
all over the world.

Kwa bahati mbaya, tiketi zake zote tatu hazikushinda! Akabaki amekata tamaa na kuendelea kushangaa kwa nini yeye hakuwa mshindi? Akaiangalia mashine ya bahati nasibu iliyomkatalia kuwa mshindi. Akaendelea kuiangalia sana kiasi cha kubaki na umbo lake kichwani, kufanya kuwa halisi kwake. Baada ya muda, alichukua umbo la mashine lililoko kichwani na kujenga mashine halisi, na ikafanya kazi!

Polisi aliyezugunda kuhusu hili na ilimshtusha mno kiasi cha kuona kuwa Reuben ana akili sana na akaamua kumpa fedha badala ya kumtoza fine kwa kuandaa michezo haramu ya Kamari! Reuben alipata fedha kutokana na mchezo wake wa bahati nasibu lakini mwishowe hakuwa na furaha. “Sikujisikia vizuri kupata fedha kuititia migongo ya watu wengine”

Alifunza kitu kimoja kuititia mapito yake: aliamini kuwa vijana wote ili kuondokana na umasikini, walihitaji kitu kimoja- ujuzi au mafunzo Fulani. Katika familia yao, wote walikuwa wafua vyuma, hivyo akaamua kurudi katika hiyo biashara. Akaihamasisha jumuiya Fulani iliyoanzishwa na kaka yake, (Kisangani Smith Group) na kuanzisha sehemu ambapo vijana wanaweza kufundishwa. Wakajifunza biashara hapo, wakitengeneza zana za kilimo maeneo jirani na wakulima.

Mmoja wao, Damian, alisema, “nilitaka kusoma na nikamuuliza Reuben kama ningeweza kufanya hivyo, akanitia moyo. Nikafanikiwa kwenda shule huku nikafanya kazi kama mfua vyuma ili niweze kujilipia masomo yangu. Elimu ni ufunguzi wa fikra na uhalisia mwinguine.”



Reuben na kikundi chake, tokea 1998 wameanzisha mradi wa upandaji miti tena katika maeneo inapokatwa kwa lengo la kufanya uuzaaji na usambazaji wa mbaao. Wanakundi wa Kikundi cha wafua vyuma Kisangani (Kisangani Smith Group) wanafanya kazi kutokana na ujuzi wanaoupata kutokana na kuwatazama wengine wafanyakyo wanapokuwa kazini. Hiyo pia iliyasaidia kuuangalizia mfereji mdogo na kuugeuza ili kutengeneza mfumo wa umwagiliaji asilia kwaajili ya shule ya chekechea ya eneo lao. Pia, bila kusubiri msaada wa serikali ambao hupitia hatua ndefu, wanakundi waliamua kuchukulia masuala mikononi mwao na kutengeneza umeme unaotumia nishati ya maji.

Mradi huu wa maendeleo kwa jamii ultokana na duka la wafua vyuma lililolenga kuwafundisha vijana. Kwa Reuben, ilikuwa kawaida kuwa kila mtu kijijini alihusishwa na kwamba waliamini kila mtu angefaidika na mradi huu. Kuna mambo mawili muhimu yaliyopelekea mafanikio hayo: uwezo wa kubuni kitu cha kiufundi kwa kutumia ujuzi asilia, kwa upande mwagine; na wakati huohuo, uwezo wa kuunganisha nguvu katika kutekeleza mradi huo.

Pamoja na Reuben kufahamu umuhimu wa kuunganisha nguvu, anamaliza kwa kusema: "Kupitia ATA Dunia ya Nnne, nimepata hamasa na ujasiri niliouhitaji. Nimeelewa kuwa, asante kwa umoja na mshikamano, kila kitu tulichopanga kufanya kinawezekana."

Semina ya Kimataifa,

June 2018

"Kilamtu Anawenza Jifunza Iwapo..."

Wajumbe wa ATD toka nchini Tanzania waliweza kushiriki semina ya kimataifa, ilioandalisha na ATD Dunia ya Nne, katika makao makuu huko Ufaransa. Dhumuni la semina hii ilikuwa ni "Kujifunza kupitia mafanikio" kwa kuonyesha ni kwa namna gani watoto wanaoishi katika hali duni ya kimaisha walivyoweza kutambua haki zao za msingi kabisa ikiwemo haki ya kupata elimu, ambayo ingaliweza kuwaongezeeza ufahamu zaidi wa jinsi ya kupata haki ya elimu kwa watoto wote ndani ya jamii. Semina hii ya kimataifa ilihusisha wajumbe mbalimbali wakiwemo Pelligia Ndimi (Mwalimu wa shule ya msingi Kunduchi), Aloyce Benjamina (Mwalimu wa shule ya msingi Pwani), Hamisi Mpanga na Laurent Ganau (Wawili hawa ni wajumbe wa kujitolea kwa muda wote katika ATD Dunia ya Nne Tanzania. Waliweza kuelezea simulizi mbalimbali za mafanikio zinazohusiana na shughuli zetu za Elimu. Miongoni mwa simulizi hizo ni "Jinsi ya kuwa mtu Fulani" ambayo ni simulizi inayomuhusu mama mmoja mpambanaji katika kuhakikisha watoto wake wanapata fursa ya kupata Elimu mashulenii, mama huyu alipata ushirikiano mkubwa kutoka shirika la ATD Dunia ya Nne pamoa na walimu.

Wajumbe kutoka takribani mataifa kumi na manne (14) katika kila bara, waliweza shirikisha simuli mbalimbali za kimafanikio katika semina. Kupitia mafunzo kwa njia ya mafanikio kwa dhana ya elimu kwa kuongeza maarifa na uzoefu kwa kundi hilo. Kupitia semina hii wajumbe waliweza kuelezea umuhimu wa wajibu wa wazazi katika kufanikisha elimu bora kwa watoto wao, pia walionyesha Kuna umuhimu Mkubwa sana wa kushirikiana baina ya wazazi, walimu na viongozi wa mamlaka ndogo ndogo za elimu kufanya kazi kwa pamoja ili kufikia lengo..

Jiweke tayari kupata uchambuzi zaidi katika Jarida linalofata...!

Darasa la wasiojua kusoma na kuandika kwa watu wazima, Tandale

Darasa la Watu Wazima la Kujifunza kusoma na kuandika bado limeendelea kuwa ni changamoto kubwa kwa Watanzania wengi hadi hii leo. Elimu ya msingi sio tu kwa ajili ya watu au kundi fulani bali ni haki ya kila mtu ndani ya Jami kupatiwa. Ndani ya jamii wazazi wengi wamekuwa wakishindwa kuweka bayana kuhusiana na jinsi watu, wakiwemo watoto wao kwamba hawakupata Nafasi ya kujifunza kusoma na kuandika kwa mfumo ulio mzuri. Hali hii inapelekeea wazazi hawa kunyanyaswa, kukandamizwa na watu wanao wazunguka ndani ya jamii katika maisha yao ya kila siku. Kama tunataka Kuona Mafanikio ya watu hawa ni lazima tuweke nguvu nyingi katika kuwapa Elimu ya watu wazima kusudi wenzetu, utu wao uweze kuheshimiwa ndani ya jamii. Eneo la Tandale jijini Dar es salaam ambapo ATD ilitoa Elimu ya kujifunza kusoma na kuandika, ilianza mwezi Septemba mpaka Decemba 2017, mafunzo haya yalihusisha kundi la watu wazima amba walikuwa tayari kujifunza bila kulazimishwa. Waliweza kutenga muda wao kwa wiki siku tatu, muda wa saa 10:00 jioni kwenda kufundishwa. Mpaka wa kozi watu wazima kumi (10) waliweza kuanza mafunzo, na watu nane (8) walifanikiwa kuhitimu mafunzo.

Miongoni mwa wanafunzi alikuwepo mfanyakazi wa mashine ya kupembua nafaka ya mahindi. Mwingine alikuwa mama wa nyumbani, ambaye alikuwa anahudumia familia kubwa na mwingine alikuwa mama aliyeblareshara ndogo ndogo wa mboga za majani katika soko kuu la Tandale. Wanafunzi waliokuwa wanakuja kusoma walikuwa wanapitia hali ngumu ya maisha, lakini licha ya changamoto za maisha ya kila siku waliweza kushiriki mafunzo ya kozi hii ya kujifunza kusoma na kuandika na mwishowe wakajua. Kwa mfano mmoja wa wanafunzi walioshiriki mafunzo haya alikuwa ni mama mjamzito, ambaye nyumbani kwake alikuwa ana watoto wawili wa kuwaangalia na kuwatimizia mahitaji yao, kila siku asubuhi. Pia mama huyu alikuwa akijishughulisha na biashara ndogo ya kupika mihogo na kuuza, akimaliza analitembeza kwa umbali Mkubwa kwa ajili ya kuiuza mihogo hiyo na kurudi mchana kuwashudumia watoto wake, na badee kujianda kwa ajili ya darasa la jioni la saa 10:00 jioni.

Baada ya Darasa la mwisho la mwezi Decemba wanafunzi walisema "wanahitaji kuendelea mbele zaidi". Hii inaonyesha kwamba kila jambo linawezekana ikiwa wanajamii toka nyanja mbalimbali watakaposikamana kwa dhati katika kufanikisha mipango mbalimbali ya kuwasadia watu wanaopitia changamoto nyingi za kimaisha katika jamii. Wanafunzi wengi walihamasika kujiendeleza kusoma zaidi, umoja na mshikamano ulizidi kuimarika mionganii mwao na kusaidiana vema katika kila jambo.

Pia wajumbe wa ATD wanaojitolea kwa muda wote waliweza kuratibu kuendesha darasa ila pasipo kujitolea vema kwa wakazi wa Tandale mambo yasingalikuwa rahisi. Kwa mfano Bibi Teddy na Ashura waliweza kukakaa na familia zao na kuwashirikisha lakini pia kuwashamasisha kushiriki katika mafunzo na kukiri wazi kuwa walipata kujifunza mengi, Bibi Teddy alisema "anafarijika na kujivunia kuwa sehemu ya marafiki wa watu wanaojifunza kusoma na kuandika kwani wamekuwa wakinishirikisha mengi yahusuyo maisha yao lakini wakati mwingine walifanikiwa analitembelea nyumbani".

Bibi Ashura alisema, mmoja wa wanafunzi nilifahamiana nae kitambo kidogo, hivyo mara nyingi nilikuwa nikimpa msaada wa kumsomea na kumsainia nyaraka zake kwa niaba yake, kwa sababu alikuwa hajui kusoma na kuandika, lakini kuna wakati ulifika sikuwa nikimwona tena akinijia kwa msaada wa kumsomea na kumsainia alikuwa anafanya mwenyewe tena kwa kujiamini, kumbe alifanya hivyo baada ya kushiriki mafunzo yatolewayo na shirika hili la ATD ya kujifunza kusoma na kuandika. Ninafuraha kubwa sana kuona mabadiliko haya kwa rafiki yangu.

Mafanikio ya Darasa la watu wazima la kujifunza kusoma na kuandika, yaliwezesha sana na uongozi toka Wizara ya elimu. Mama Mtasingwa, ambaye alikuwa mhusika mkuu wa mpango wa Elimu kwa watu wazima katika wilaya ya Kinondoni, alijitahidi sana akishirikiana na wafanyakazi wenzake katika kutafuta walimu pamoja na shule zitakazowapokea watu wazima. Kwa namna ya pekee shule ya msingi Tandale ilifungua mlango wenye upendo kwa kutengeneza mazingira mazuri na rafiki kwa wanafunzi kujifunza, pia kwa kushirikiana na uongozi wa serikali ndogo ndani ya mtaa wa Tandale tuliweza kuanzisha darasa.



Aidha kutokana na uzoefu huu, uongozi wa shule ya msingi Tandale wanatarajia kuanzisha Darasa jipyaa la mafunzo kwa watu wazima huko mbeleni. Hii itakuwa fursa ya kuendeleza na kuwakaribisha watu wazima ndani ya jamii wapya na wale walokwisha jiunga tayari kushiriki mafunzo, na hata hivyo kuwashirikisha wanafunzi walifanikiwa kupata mafunzo haya kuweza kuandaa vema mafunzo kwa watu wazima.

"Nilikuwa na shangaa saana kwa mtu mzima kama mimi kuweza kujifunza, lakini sasa naweza kusoma na kuandika mwenyewe taratibu. Ninajisifu sana juu ya hili. Mjukuu wangu alinisaidia." - Bibi Arafati